FoodLAND

(Food and Local, Agricultural and Nutritional Diversity)

Kilimo Chakula Asilia na Lishe Anuwai

Kwa ufadhili wa euro milioni saba, washiriki wa nchi za Afrika na Ulaya wanaendesha mradi wa kimataifa wa kuboresha lishe na mifumo asilia ya chakula katika nchi za Afrika. Mradi huu, kwa kifupi "FoodLAND" unazinduliwa katika mkutano wa kimtandao kuanzia tarehe 30 Septemba mpaka tarehe 2 Oktoba, 2020.

Jumla ya washiriki 28 wenye utaalamu mbalimbali wataunganika pamoja na kuhudhuria mkutano huo kwenye tarehe zilizotajwa hapo mwanzo.. Mkutano huu utafanyika kwa njia ya kimtandao kutokana na ugonjwa wa korona (COVID-19) ambalo ni janga la dunia. Mradi wa FoodLAND umepata ufadhili wa euro millioni saba kutoka kwa Kamisheni ya Ulaya (*European Commission*) kupitia programu ya "Horizon 2020" na unaoratibiwa na Alma Mater Sutudiorum, kampusi ya Chuo Kikuu cha Bologna kilichoko nchini Italia.

Mradi huu utajikita katika kutengeneza bunifu mbalimbali zinazohusiana na maendeleo ya kilimo na ufugaji wa samaki na kuwashauri walaji kuhusu tabia ya ulaji wa chakula kwa afya njema katika nchi sita za Afrika. Nchi hizo ni Morocco,Tunisia, Ethiopia, Kenya, Uganda na Tanzania. Kwa ujumla lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha baiyoanuwai katika kilimo (*Agrobiodiversity*) na utumiaji wa aina mbalimbali za chakula pamoja na matumizi ya aina mbalimbali za mlo kwa ajili ya afya njema ili kupambana na utapiamlo katika nchi hizi za Afrika.

Mradi huu utaunda mtandao wa vitovu vya chakula (*local food hubs*)14 kwenye wilaya/vijiji ambazo zitafungamanishwa na miji 14 kwenye hizo nchi ambazo zitawaunganisha watendaji kutoka vijijini, mjini na sehemu zilizokandokando na miji kuwa kama mahali pa kuzijaribu na na kuanza kuzitumia bunifu zitatazotokana na mradi huu. Washiriki 28 katika mradi huu wanaounda muungano wa FoodLAND (*Consortium*) (18 ni kutoka nchi za Afrika na 10 kutoka nchi za bara la Ulaya) watafanya kazi wakishirikiana pamoja kutengezeza/kuunda, kutekeleza na kuthibitisha utaalamu na tekinolojia 12. Utaalamu na tekinolojia hizo zitakuwa ni miundo na tekinologia za mbogamboga, ufugaji wa samaki na usindikaji wa vyakula pamoja na utengenezaji wa aina mpya 17 za vyakula mbalimbali. Vyakula hivyo vitakuwa mbogamboga na samaki ghafi (fresh), zilizokaushwa na zilizosindikwa, ukaushaji na usindikaji wa mbogamboga na samaki kutengenezea unga mchanganyko pamoja na vyakula tiba (*therapeutic foods*).

Mradi wa FoodLAND unatumia utaratibu wa kuwahusisha wadau kuanzia chini kwenda juu yaani kujali mahitaji na mapendekezo, mahitaji na uchaguzi wa wazalishaji na walaji. Mradi utajitahidi kupata picha halisi ya mahitaji ya lishe ya wakazi wa kwenye miji mikubwa na vijijini, pia kuelewa hali ya kiuchumi, mazingira ya uzalishaji na sababu zinazopelekea wakulima na wasindikaji wadogo kufanya maamuzi wanayoyafanya. Wakulima wadogo na waendeshaji wa sehemu za huduma za chakula watapokea msaada/ushauri utakaohamasisha kujali lishe bora na uzalishaji wa mazao tofauti ya kilimo. Wakati huohuo walaji watashiriki katika kampeni za kuongeza uelewa na mawasiliano

FOODLAND has received funding from the European Union's Horizon 2020 research and innovation programme under grant agreement (GA No 862802).
The views and opinions expressed in this document are the sole responsibility of the author and do not necessarily reflect the views of the European Commission.

kuhusu lishe bora. “Kwa kuziba pengo kati ya uzalishaji na matumizi ya vyakula, mradi utaimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula na mnyororo mzima wa upatikanaji wa chakula na hii itatengeneza fursa ya masoko ndani na nje ya nchi” Hii imesemwa na Marco Setti, Professor wa Kilimo na Chakula wa Chuo Kikuu cha Bolgna ambaya ni Mratibu Mkuu wa mradi huu.

Mawasiliano

Email: info@foodland-africa.eu
Tovuti/Website: www.foodland-africa.eu | Follow #FoodLANDAfrica
@FoodLANDafrica on Twitter and Facebook | FoodLAND-Africa on LinkedIn
Maelezo ya ziada katika CORDIS: https://cordis.europa.eu/project/id/862802

FOODLAND has received funding from the European Union’s Horizon 2020 research and innovation programme under grant agreement (GA No 862802).
The views and opinions expressed in this document are the sole responsibility of the author and do not necessarily reflect the views of the European Commission.

The FoodLAND consortium

Research partners: **(WASHIRIKI WA UTAFITI)**

Alma Mater Studiorum - Università Di Bologna (Coordinator), Italy
Agroscope, Switzerland
The James Hutton Institute, UK
Copenhagen Business School, Denmark
Ecole Nationale d'Agriculture de Meknes, Morocco
Institut Supérieur Agronomique de Chott-Mariem, Tunisia
Institut National Agronomique de Tunisie, Tunisia
Mekelle University, Ethiopia
University of Nairobi, Kenya
Sokoine University of Agriculture, Tanzania
Makerere University, Uganda
National Agricultural Research Organisation, Uganda

Partners for agriculture/aquaculture promotion and sustainable development in Africa

WASHIRIKA WA KUKUZA KILIMO / UFUGAJI WA SAMAKI NA MAENDELEO ENDELEVU BARANI AFRIKA

Ethiopian Agricultural Transformation Agency Tigrai, Ethiopia
Ministry of Agriculture Livestock and Fisheries, Kenya
Comitato Europeo per la Formazione e l'Agricoltura, Italy
Relief Society of Tigray, Ethiopia
Volunteer Efforts for Development Concerns, Uganda
Farm Concern International, Kenya
Helvetas Tanzania, Switzerland
Groupement d'Intérêt Economique Zoyout Dir Béni Mellal, Morocco
Groupement de développement agricole Hrayer Gloub thiran, Tunisia

Small and medium-sized companies in the food sector

KAMPUNI NDOGO NA ZA KATI KATIKA SEKTA YA CHAKULA

Kitui Enterprise Promotion Company Limited, Kenya
Tamarillo Kenya Limited, Kenya
Katundu Traders Limited, Tanzania
Nutreal Limited, Uganda
AquaBioTech Limited, Malta

Industrial partner

MSHIRIKA WA VIWANDA

Novamont S.p.A, Italy

Communication and IPR management partners

FOODLAND has received funding from the European Union's Horizon 2020 research and innovation programme under grant agreement (GA No 862802).
The views and opinions expressed in this document are the sole responsibility of the author and do not necessarily reflect the views of the European Commission.

MAWASILIANO NA WASHIRIKA WA USIMAMIZI WA IPR

Elhuyar Fundazioa, Spain
EURICE, Germany

FOODLAND has received funding from the European Union's Horizon 2020 research and innovation programme under grant agreement (GA No 862802).
The views and opinions expressed in this document are the sole responsibility of the author and do not necessarily reflect the views of the European Commission.